

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma haina Utani katika Mapato

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imeendelea na jitihada za makusudi ili kuhakikisha wananchi na wakazi wake wanafanikisha malengo yao ya kujiletea maendeleo. Jitihada hizi kwa kiasi kikubwa zinachagizwa na kauli mbiu ya Serikali ya awamu ya tano maarufu kama "Hapa kazi tu".

Ikumbukwe kuwa mwaka 2015 waziri Mkuu wa Tanzania akiwa Mkoani Dodoma Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa akiwahutubia Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya katika kilele cha Mkutano Mkuu wa Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) alitoa agizo kwa Halmashauri zote nchini kuwa Halmashauri yoyote ambayo haitafikisha asilimia 80 ya mapato ya ndani itafutwa.

Hotuba ya Waziri mkuu ilichukuliwa katika mitazamo tofauti katika kona zote za Taifa hili lililojaliwa kila aina ya Utajiri. Kwa wengine agizo hili lilichukuliwa kama onyo kwa halmashauri wakati wengine lilijenga hisia za uwekaji mikakati ili kuondoka katika mtego katika mtego wa kufutwa.

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni miongoni mwa Halmashauri za Manispaa ambazo kwa muda wa miaka kadhaa iliyopita ilikuwa ikikusanya mapato yake ya ndani chini ya asilimia 90. Kwa mfano kwa mwaka 2015/2016 Halmashauri ilikusanya asilimia 82. Makisio ya Mapato ya ndani yalikalidiriwa kuwa 2,145,947,100 kiasi kilichokusanywa kilikuwa 1,779,017,447.39 sawa na asilimia 82.90

Pamoja na makusanyo hayo ya kulidhisha bado halmashauri ya Manispaa ya Musoma iliendelea na jitihada za kuongeza mapato yako kwa kuweka mikakati madhubuti ya kukusanya mapato hayo.

Miongoni mwa jitihada za makusudi zilizochukuliwa ni pamoja na matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji pamoja na kuweka malengo ya ukusanyaji kwa kila wakala. Jitihada hizi zimezaa matunda ambapo kwa kwaka 2016/2017 halmashauri ilivuka lengo kwa kukusanya asilimia 103.65

ambapo makisio yalikuwa Tsh. **1,634,773,000.00** na mpaka kufikia Juni 30 2017 kiasi kilichokusanywa kilikuwa Tsh. **1,694,508,366.32**.

Katika mafanikio ya makusanyo hayo vyanzo vilivyofanya vizuri vilikuwa pamoja na ada za Leseni za Biashara, Ushuru wa Machinjio, Ushuru wa samaki na dagaa, ada ya Leseni za vileo pamoja na Ushuru wa matangazo. Aidha, chanzo kingine kilichofanya vizuri ni Leseni za Mitumbwi.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Musoma akitoa maoni kuhusu makusanyo ya Halmashauri kwa mwaka 2016/2017 anasema ushirikiano mkubwa uliooneshwa na wataalamu wa Manispaa pamoja na usimamizi madhubuti wa Baraza la Madiwani.

“Mwaka ulipoanza tuligundua lazima tuweke mikakati ya ukusanyaji kwa kuwataka wataalamu waweke mikakati ya ukusanyaji ambapo baada ya kila mtu kutimiza wajibu tumefanikiwa kwa mara ya kwanza kuvuka lengo” anasema Mhe. William Gumbo.

Mhe. Gumbo anaongeza kuwa tamko la Serikali kwa mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinakusanya juu ya asilimia 80 liliziasha Halmshauri nyingi nchini na matunda ya tamko hilo yanaonekana bayana.

Aidha Mhe. Gumbo anasisiza kuwa “bado zipo jitihada za makusudi zinahitaji kuchukuliwa ili kuziba mianya yote katika makusanyo ya mapato ya Serikali.Matarajio yetu ni kuendelea na mapambano ili kufikia malengo na kuwaletea maendeleo wakazi wa Manispaa ya Musoma”.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma Bi. Fidelica Myovella anasema “Siku zote jitihada na ushirikiano unalipa, makusanyo haya yaliyokusanywa yanatutia moyo sana na kutupa ujasiri wa kufanya vizuri zaidi kwa mwaka wa fedha ujao” anasema.

“Tunaendelea kuongeza vyanzo va mapato ili kupanua wigo wa Halmashauri kujitegemea na kuongeza uwezo wa Halmashauri kutoa huduma kwa wananchi” anasema Bi. Myovella.

Vyanzo vipya vinavyotajwa kuongezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni pamoja na chanzo cha madini ya ujenzi pamoja na chanzo cha vibali vya ujenzi.